

Siku 16 za Uanaharakati za Kupinga Ukatili wa Kijinsia mwaka wa 2026

Muhtasari wa Kampeni

1. Usuli wa Kampeni

Tangu mwaka wa 1991, kampeni ya **Siku 16 za Uanaharakati za Kupinga Ukatili Wa Kijinsia (UWAKI)** zimeunganishwa na vuguvugu za uanaharakati, wanaharakati, mashirika, jamii na washirika mbalimbali ili kupinga ukatili dhidi ya wanawake na wasichana na kukuza usawa na usalama. Tangu mwaka wa 2004, Mtandao wa Kuzuia Ukatili wa Kijinsia umewasaidia wanachama wake kushiriki katika kampeni hiyo na kuimarisha juhudi za pamoja za kuzuia ukatili dhidi ya wanawake katika kanda.

Mwaka huu wa **2026**, kazi ya kuzuia ukatili dhidi ya wanawake inaendelea huku tukishuhudia nafasi ya kiraia ikipungua, uwanda wa mtandaoni wenye sumu, taarifa potofu, simulizi zenye kupinga haki za binadamu, upungufu wa ufadhili, na shinikizo kubwa kwa uanaharakati. Hata katika mazingira haya magumu, mashirika ya haki za wanawake, wanaharakati, wahanga, na jamii wanaendelea kujipanga, kukabiliana ili kuleta mabadiliko.

Dhidi ya hali hii, kampeni inatuhimiza **tutengeneze upya mamlaka yetu** kwa pamoja kwa kuimarisha mshikamano, kujijali, ubunifu na kuchukua hatua ya kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake na **kutengeneza mustakabali wa baadae: bila ukatili, hofu na ubaguzi.**

2. Dhamira ya Kampeni ya mwaka 2026

“Tengeneza Upya Mamlaka Yetu:
Hatua za pamoja kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake”

Kauli Mbiu: Wezesha. Chukua Hatua. Tengeneza Mustakabali wa Baadae.

Kauli mbiu ya mwaka wa 2026 inatambua kuwa **Ukatili Dhidi ya Wanawake unatokana na mahusiano yasiyo na usawa ya mamlaka.** Hivyo, tunahitaji kuzuia zaidi kuliko kutoa huduma baada ya vitendo vya ukatili kutokea; tunahitaji kuchukua hatua endelevu za kubadilisha kanuni zitokanazo na mila, mahusiano, taasisi na mifumo inayochochea ukatili na kutokuwepo na usawa.

Wakati wimbi la upinzani dhidi ya usawa wa kijinsia likichangia uwepo wa changamoto mbalimbali na kuminywa kwa ushiriki wa kiraia, kudhoofisha vuguvugu za uanaharakati, na kubana rasilimali za kuzuia. ni jambo la dharura zaidi kwa wakati huu kutengeneza upya mamlaka yetu inayochochea mabadiliko.

Kutengeneza upya mamlaka yetu maana yake ni kujiunganisha tena na kusudi letu, maarifa, mahusiano, uongozi, ubunifu, na nguvu ya pamoja. Jitihada za kuzuia ukatili huendelezwa si kwa watu binafsi wanaofanya kazi peke yao, bali kwa jamii, vuguvugu la uanaharakati, mashirika, na washirika kuchukua hatua za pamoja.

Kwa hivyo kampeni inatuhimiza tufanye yafuatayo:

a. **Tujijengee uwezo** sisi wenyewe na wengine kwa kuimarisha uwakala, uongozi, maarifa na kupaza sauti kwa pamoja.

b. **Tuchukue hatua** kwa pamoja ili kupinga kanuni potofu zitokanazo na mila, mahusiano yasiyo na usawa katika mamlaka, na kukataa upinzani.

c. **Kutengeneza mustakabali wa baadae** kwa kutumia ubunifu na maono yenye ujasiri, kuwekeza katika vuguvugu za uanaharakati wa kifeministi, kuzuia, kujaliana, mshikamano na mazingira yanayohitajika kwaajili ya mabadiliko ya kudumu.

3. Malengo ya Kampeni

Kampeni ya mwaka 2026 ina malengo makuu manne:

a. Kuchochea hatua za kutengeneza upya nguvu na mamlaka yetu katika ngazi ya mtu binafsi, taasisi, na jamii kwa ujumla.

b. Kukuza ushirikiano wenye tija unaozingatia zaidi juhudi za kuzuia ukatili dhidi ya wanawake.

c. Kuchochea mitazamo mipya ya kifikra, kuleta matumaini, na ujasiri ili kutengeneza mustakabali wa juhudi za kuzuia ukatili dhidi ya wanawake.

4. Ujumbe Mkuu wa Kampeni

Mamlaka yetu yanatokana na umoja, na tuna jukumu la kutengeneza mustakabali wetu wenyewe. Tunatengeneza upya mamlaka yetu kwa kujaliana, kujipanga, kupinga kanuni potofu zitokanazo na mila, kuchagiza ubunifu, na kuwekeza zaidi kwenye vuguvugu za uanaharakati zilizo imara na zenye ustahimilivu. Kwa pamoja, tunaweza kukabiliana na changamoto zitakazojitokeza, kuibua fursa mpya na kutengeneza mustakabali wa baadae ambao wanawake na wasichana wataishi bila ya ukatili.

Wezesha. Chukua Hatua. Tengeneza Mustakabali wa Baadae.

5. Jinsi Wadau Wanavyoweza Kushiriki

Wanachama wa Mtandao wa Kuzuia Ukatili wa Kijinsia, wadau wa vyombo vya habari na washirika wanaweza kuunga mkono kampeni kwa kuchukua hatua zifuatazo:

a. **Kupaza sauti ya pamoja:** Tumia dhamira na kauli mbiu kuinua ufeministi, wahanga, na sauti ya jamii, uzoefu wetu, ili kuleta suluhisho na uongozi.

b. **Hamasisha hatua za pamoja:** Tengeneza nafasi kwaajili ya mazungumzo, andaa na kuchukua hatua ya kupinga kutokuwepo na usawa wa mamlaka, kanuni potofu zitokanazo na mila, na mifumo inayoendeleza Ukatili wa Kijinsia.

c. **Tengeneza mustakabali wa baadae:** Tumia simulizi za hadithi, vyombo vya habari, ubunifu na majukwaa yatakayo jitokeza ili kutafakari na kujenga mustakabali wa baadae ambao wanawake na wasichana wataishi bila ya ukatili.

d. **Imarisha vuguvugu la uanaharakati na mshikamano:** Jenga ushirikiano katika mashirika, watu wa rika mbalimbali, jamii na mataifa mbalimbali huku ukihamasisha kujaliana kwa pamoja, usalama na ustahimilivu.

e. **Wekeza katika kuzuia kwa njia endelevu:** Fanya utetezi kuhusu rasilimali, uongozi na kujitoa kwa muda mrefu kutakako pelekea kugeuza kasi ya kampeni kuwa mabadiliko ya kudumu.

6. Wito wa Kuchukua Hatua

Kwa Watu Binafsi: Tengenezeni upya mamlaka yenu. Chukueni hatua kwa pamoja.

i. Tafakari na utambue njia zinazorejesha nguvu zako, matumaini na ujasiri: tenga muda wa kujijali, tafakari, na shiriki katika mazungumzo na watu wenye mitazamo sawa na wewe ili kubadilishana mawazo kuhusu hali ya wakati huu na mwelekeo wa kuzuia ukatili dhidi ya wanawake.

ii. Shiriki katika kuchukua hatua zinazopinga kanuni potofu zitokanazo na mila, paza sauti dhidi ya ukatili dhidi ya wanawake, waunge mkono wahanga kwa kuzingatia utu, na paza sauti yako katika majukwaa ili kuimarisha mshikamano na juhudi za kuzuia ukatili.

Kwa Jamii: Andaa, Jali na Lete Mabadiliko

i. Tengeneza nafasi ambayo wanawake na wasichana wanaweza kushiriki na kuongoza. Pinga vitendo vinavyoweza kusababisha ukatili na jenga mitandao ya kujijali, uwajibikaji na kuchukua hatua za pamoja zinazodumisha kuzuia ukatili hata baada ya kampeni ya Siku 16.

Kwa Mashirika: Jenga ustahimilivu na tengeneza mustakabali wa baadae

i. Waalike wafanyakazi na wadau kwa pamoja ili kufanya uchambuzi wa jinsi wanavyoweza kutengeneza upya mamlaka ya pamoja ndani ya mashirika yao na wadau wao, ili kuimarisha uwezo wao wa kukabiliana vyema na fursa na changamoto za kipindi hiki, na kutambua hatua zinazoweza kuchukuliwa.

Kwa wafadhili na watunga sera: Tengeneza Masharti kwaajili ya Kuzuia Ili kuleta Kustawi

i. Wekeza katika taarifa zinazozingatia Ushahidi, mkakati wa kuzuia unaoongozwa na jamii; linda nafasi za kiraia; shughulikia vichocheo vya kimuundo vinavyosababisha ukatili dhidi ya wanawake; na shirikisha kwa njia madhubuti mashirika yanayoongozwa na wanawake na ya kifeministi katika kuandaa sera, mifumo na kuleta suluhisho la muda mrefu.

7. Kauli Mbiu ya Kampeni

Wezesha. Chukua Hatua. Tengeneza Mustakabali Wa Baadae.

- **Wezesha:** Imarisha uwezo wa uwakala, uongozi, maarifa, mahusiano na sauti ya pamoja.
- **Chukua Hatua:** Geuza mshikamano kuwa hatua endelevu zinazozuia ukatili na kubadilisha mifumo ya mamlaka isiyo na usawa.
- **Tengeneza mustakabali wa baadae:** Jenga jamii, vuguvugu la uanaharakati, taasisi na mifumo ambayo wanawake na wasichana wanaweza kuishi kwa kuheshimu utu, usalama, usawa na bila kuwepo na ukatili.

8. Jiunge na Kampeni ya Siku 16 ya Mwaka wa 2026

Toleo la mwaka wa 2026 la kampeni ya Siku 16 linatoa wito wa **kutengeneza upya mamlaka yetu**, **kuimarisha mahusiano yetu, na kuchukua hatua kwa pamoja.** Kuanzia tarehe **25 Novemba hadi 10 Desemba 2026,** tutumie sauti zetu kwa pamoja, majukwaa, uhusiano, ubunifu na rasilimali zetu ili kuendeleza juhudi za kuzuia na kujenga mustakabali wa baadae usio na ukatili dhidi ya wanawake.

#RenewOurPower | #EmpowerActShapeTheFuture | #16DaysOfActivism | #PreventVAW | #CollectiveAction